# HALMASHAURI YA WILAYA YA BAGAMOYO

## MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO KILICHOFANYIKA TAREHE 29/10/2021 KWENYE UKUMBI WA MIKUTANO WA SHULE YA MSINGI MWAMBAO

### WAJUMBE WALIOHUDHURIA:

| | | | |
|---|---|---|---|
| 01: | Diwani M. A. Usinga | - | Mwenyekiti |
| 02: | Diwani C.D. Chandika | - | Makamu Mwenyekiti |
| 03: | Diwani S. A. Ngatipura | - | Mjumbe |
| 04: | Diwani S. R. Honello | - | Mjumbe |
| 05: | Diwani A.M. Pyalla | - | Mjumbe |
| 06: | Diwani A. A. Issa | - | Mjumbe |
| 07: | Diwani U.M. Kisebengo | - | Mjumbe |
| 08: | Mh. Muharami Mkenge (MB) | - | Mjumbe |
| 09: | Ndg. Shauri Selenda | - | Mkurugenzi Mtendaji (W) – Katibu |

### WATAALAM WALIOHUDHURIA:

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 01: | Ndg. | Mwalukasa, G.A. | - | Afisa Utumishi/Utawala (W) |
| 02: | Ndg. | Mzeru, G. | - | Mweka Hazina (W) |
| 03: | Ndg. | Wilson, B. | - | Kny. Mwanasheria (W) |
| 04: | Ndg. | Mhina, M.S. | - | Mkuu wa Kitengo cha Misitu/Nyuki |
| 05: | Ndg. | Nziku, E | - | Kaimu Afisa Kilimo/Umwagiliaji (W) |
| 06: | Ndg. | Shindai, P.M. | - | Mkaguzi wa Ndani (W) |
| 07: | Ndg. | Ndimbe, N. | - | Afisa TEHAMA |
| 08: | Ndg. | Mporere, E. | - | Kaimu Afisa Elimu Sekondari (W) |
| 09: | Dr. | Masunga, K | - | Kaimu Afisa Mifugo na Uvuvi (W) |
| 10: | Ndg. | Stili, A. | - | Afisa Mtendaji Mkuu M/Mji |
| 11: | Ndg. | Urassa, T. | - | Afisa Uchaguzi (W) |
| 12: | Ndg. | Kapinga, M.M. | - | Afisa Mipango (W) |
| 13: | Ndg. | Nteye, A.S | - | Afisa Ugavi na Manunuzi (W) |
| 14: | Ndg. | Mahilane, D. | - | Mratibu wa TASAF H/W |
| 15: | Ndg. | Kwayu, F | - | Kaimu Afisa Elimu Msingi (W) |
| 16: | Dr. | Mwakipesile | - | Mganga Mkuu (W) |
| 17: | Ndg. | Shabani, H. | - | Kaimu Afisa M/Jamii (W) |
| 18: | Ndg. | Fulgence, K | - | Kaimu Afisa Hifadhi ya Mazingira |
| 19: | Ndg. | Masanja, F | - | Kaimu Afisa Ardhi na Maliasili (W) |
| 20: | Ndg. | Sikutegemea, P | - | Kaimu Mhandisi wa Ujenzi (W) |

*KATIBU:............................*        *M/KITI:............................*

**WAKARIBISHWA:**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 01: | Ndg. Gladness Shafii | - | Afisa Tarafa Yombo |
| 02: | Ndg. Dorice Mwakatobe | - | Afisa Tarafa Mwambao |

**SEKRETARIETI:**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 01: | Ndg. Katikiro, P.M | - | CC |

**MUHT.NA.HWB/FUM/05/64/2021/2022 - KUFUNGUA KIKAO**

Mkurugenzi Mtendaji (W) ambaye pia ndiye Katibu wa Kikao hiki, alianza kwa kuwafahamisha Wajumbe kuwa, Kikao hicho kilikuwa ni Kikao cha kawaida cha Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango mahususi kwa ajili ya maandalizi ya Mkutano wa Baraza la Madiwani kwa kipindi cha Julai, 2021 hadi Septemba, 2021 - robo ya kwanza ya mwaka 2021/2022.

Katika Kikao hiki Wajumbe walipokea na kujadili Taarifa ya Fedha, Mapato na Matumizi kwa kipindi cha mwezi Septemba, 2021 ikiwa ni taarifa ya mwaka 2021/2022 sambamba na kupokea taarifa mbalimbali kuhusiana na Uendeshaji wa shughuli mbalimbali katika Halmashauri ya Wilaya Bagamoyo kwa kipindi cha Julai, 2021 hadi Septemba, 2021 - robo ya kwanza ya mwaka 2021/2022.

Baada ya Mkurugenzi kutoa maelezo hayo ya utangulizi alimkaribisha Mwenyekiti kufungua Kikao hicho.

Mwenyekiti aliwakaribisha Wajumbe wote waliohudhuria katika Kikao hicho, aidha aliwasihi kushirikiana katika kujadili Agenda zilizoandaliwa ili hatimaye kuweza kutoa maoni na ushauri kwa lengo la kuboresha taarifa hizo kabla ya kuwasilishwa kwenye Mkutano wa Baraza la Wah. Madiwani kwa hatua za kuridhiwa kwa ajili ya kuendelea na utekelezaji kama ilivyokusudiwa

Mwenyekiti alikifungua Kikao mnamo saa 5.50 asubuhi.

**MUHT.NA.HWB/FUM/05/65/2021/2022 - KUTHIBITISHA AGENDA ZA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO CHA TAREHE 29/10/2021**

Kikao kiliwasilishiwa na kusomewa Agenda za Kikao cha Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango cha tarehe 29/10/2021 kama ifuatavyo: -

01: Kufungua Kikao

02: Kuthibitisha Agenda za Kikao cha Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango cha tarehe 29/10/2021

03: Kusoma na Kuthibitisha Muhtasari wa Kikao cha Kamati ya Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango cha tarehe 27/09/2021 (Maalum – Final Acct), tarehe 28/09/2021 (kawaida) na tarehe 29/09/2021 (kawaida)

04: Yatokanayo na Muhtasari wa Kikao cha Kamati ya Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango cha tarehe 28/09/2021 na tarehe 29/09/2021

05: Kuwasilisha utekelezaji wa maagizo/maazimio yaliyotolewa kwenye Mkutano wa Baraza la Madiwani robo ya nne ya mwaka 2020/2021

06: Taarifa ya Fedha, Mapato na Matumizi kwa kipindi cha mwezi Septemba, 2021 kwa mwaka 2021/2022

07: Taarifa ya Mapokezi ya Fedha kwa mwezi Septemba 2021

08: Taarifa ya Ziara ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kwa kipindi cha Julai, 2021 hadi Septemba, 2021 – robo ya kwanza 2021/2022

09: Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa kipindi cha Julai, 2021 hadi Septemba, 2021 – robo ya kwanza 2021/2022

10 Taarifa ya Ukaguzi wa Ndani kwa Hesabu za Halmashauri ya Wilaya kwa kipindi cha Julai , 2021 hadi Septemba, 2021 – robo ya kwanza 2021/2022

11: Taarifa ya Shughuli za Bodi ya Zabuni ya H/Wilaya kwa kipindi cha Julai - Septemba, 2021 – robo ya kwanza ya 2021/2022

12: Taarifa ya Manunuzi yaliyofanyika katika Halmashauri ya Wilaya kwa kipindi cha Julai - Septemba, 2021 – robo ya kwanza ya 2021/2022

13: Taarifa ya Utekelezaji wa Vihatarishi vya Halmashauri ya Wilaya kwa kipindi cha Julai - Septemba, 2021 – robo ya kwanza ya 2020/2021

14: Taarifa za Utendaji Kazi na Utekelezaji wa shughuli Mbalimbali kwa Idara/Vitengo vya Utawala kwa kipindi cha Julai - Septemba, 2021 – robo ya kwanza ya 2021/2022 kutoka:

- Idara ya Mipango, Ufuatiliaji na Takwimu
- Idara ya Fedha na Biashara
- Idara ya Utumishi na Utawala
- Kitengo cha Sheria
- Kitengo cha Manunuzi na Ugavi
- Kitengo cha TEHAMA
- Kitengo cha Uchaguzi
- Mamlaka ya Mji Mdogo Bagamoyo

*KATIBU:..............................* *M/KITI:............................*

15: Mgao wa fedha **Tshs. 43,566,953.37 /=** za Mapato ya Ndani kwenda Miradi ya Maendeleo kwa kipindi cha mwezi Septemba, 2021

16: Kuwasilisha Taarifa ya Utoaji wa Mikopo kwa Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu awamu ya kwanza ya mwaka 2021/2022

17: Taarifa ya Mapokezi ya Fedha kutoka OR – TAMISEMI kiasi cha Tshs. 300,000,000/= kwa ajili ya Ujenzi wa Jengo la Dharura katika Hospitali ya Wilaya Bagamoyo

18: Taarifa ya Mapokezi ya Fedha na Mpango kazi wa Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyopokea Fedha kutoka Serikali Kuu kwa Sekta za: Elimu Sekondari, Elimu Msingi na Afya

19: Taarifa ya idadi ya majengo yatakayojengwa katika KItuo cha Afya Fukayosi

20: Taarifa ya Ujenzi wa Nyumba moja ya Watumishi 3 in 1 yenye uwezo wa kuchukuwa familia tatu 3

21: Taarifa ya Uchunguzi/Ukaguzi uliofanywa na Taasisi ya TAKUKURU kuhusiana na deni la Mkandarasi M/S Mzinga Holdings Co. Ltd kuhusu ujenzi wa vyumba 17 vya maabara

22: Gharama kwa ajili ya ukamilishaji wa ujenzi wa Nyumba ya Mganga katika Zahanati ya Kaole katika Kata ya Dunda

23 Taarifa ya Hatua za Utekelezaji wa Mradi Mkakati wa Ujenzi wa Soko la Kisasa la Samaki Bagamoyo

24: Kupitisha na Kuidhinisha Rasimu ya Sheria Ndogo za Halmashauri ya Vijiji vilivyopo katika Kata ya Yombo na Kata ya Fukayosi

25: Kupitisha na Kuidhinisha Rasimu za Sheria Ndogo ya Halmashauri ya Wilaya Bagamoyo za mwaka 2021

26: Kuwasilisha Utaratibu wa kuwapanga Wamachinga katika maeneo ya H/Wilaya Bagamoyo kwa ajili ya kufanya biashara zao

27: Mpango kazi wa Utekelezaji wa Mikakati ya Ukusanyaji wa Mapato kwa mwaka 2021/2022 kutoka Idara/Vitengo vya H/Wilaya Bagamoyo

28: Taarifa ya chanzo cha Zabuni ya Ushuru wa Mazao ya Misitu

29: Maombi ya Kibali cha kutangaza nafasi ya Mwenyekiti wa Bodi ya Ajira ya H/Wilaya baada ya Mwenyekiti aliyekuwepo sasa kumaliza muda wake

*KATIBU:.............................* *M/KITI:............................*

30: Taarifa ya kupatikana kwa Mtaalam wa muda wa Mionzi katika Hospitali ya Wilaya na maombi ya kibali cha Ajira ya muda

31: Maombi ya Kibali cha kuajiri Watumishi wa muda watatu (3) wa Kada ya Ujenzi

32: Maombi ya Kibali cha kulipa malipo kwa Vibarua wa kukusanya Mapato waliomaliza muda wao baada ya kubinafsisha na Kibali cha kuendelea na Vibarua wa Mapato katika maeneo yasiyobinafsishwa

33: Taarifa ya Uteuzi wa Wajumbe Wapya wa Bodi ya Zabuni ya H/Wilaya Bagamoyo

34: Taarifa ya kupatikana kwa Kibali cha Ajira ya Afisa Mteknolojia Drj. II

35: Kufunga Kikao

Wajumbe walizipokea Agenda hizo, kisha kwa pamoja walizipitisha kuwa ni agenda sahihi kwa ajili ya kujadiliwa katika Kikao cha Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango cha tarehe 29/10/2021 kama zilivyowasilishwa.

**MUHT.NA.HWB/FUM/05/66/2021/2022 - KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO CHA TAREHE 27/09/2021 (MAALUM – FINAL ACCT), TAREHE 28/09/2021 (KAWAIDA) NA TAREHE 29/09/2021 (KAWAIDA)**

Kikao kiliwasilishiwa na kusomewa Muhtasari wa Kikao cha Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango kilichofanyika tarehe 27/09/2021 (Maalum – Final Acct), tarehe 28/09/2021 (Kawaida) na tarehe 29/09/2021 (Kawaida), Wajumbe waliipokea Mihutasari hiyo na Kisha waliiithibitisha kuwa ni kumbukumbu sahihi za Vikao hivyo.

**MUHT.NA.HWB/FUM/05/67/2021/2022 - YATOKANAYO NA MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO CHA TAREHE 27/09/2021 (MAALUM – FINAL ACCT), TAREHE 28/09/2021 (KAWAIDA) NA TAREHE 29/09/2021 (KAWAIDA)**

Kikao kiliwasilishwa na kusomewa utekelezaji wa maagizo/maazimio yaliyotolewa kwenye Kikao cha Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango kilichofanyika tarehe tarehe 27/09/2021 (Maalum – Final Acct), tarehe 28/09/2021 (Kawaida) na tarehe 29/09/2021 (Kawaida), kama ifuatavyo:-

*KATIBU:............................* *M/KITI:...........................*

**USHAURI:**

Idara ya Afya kwa kushirikiana na Idara ya Ujenzi mara baada ya kuwasilishwa kwa mchoro wa ujenzi wa jengo la dharura kutoka OR – TAMISEMI wafanye tathmini na kujiridhisha kama jengo la dharura lililopo katika Hospitali ya Wilaya linafanana na mchoro utakaowasilishwa kutoka OR – TAMISEMI

**MAKUBALIANO**

01: Wajumbe wa Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango wote kwa pamoja waliipitisha taarifa ya mapokezi ya Tshs. 300,000,00/= kutoka OR – TAMISEMI kwa ajili ya ujenzi wa jengo la dharura katika Hospitali ya Wilaya Bagamoyo kuwa ni taarifa sahihi kama ilivyowasilishwa

02: Taarifa ya mapokezi ya Tshs. 300,000,00/= kutoka OR – TAMISEMI kwa ajili ya ujenzi wa jengo la dharura katika Hospitali ya Wilaya Bagamoyo iwasilishwe kwenye Mkutano wa Baraza la Madiwani ujao

**MUHT.NA.HWB/FUM/05/81/2021/2022 - TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA NA MPANGO KAZI WA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOPOKEA FEDHA KUTOKA SERIKALI KUU KWA SEKTA ZA: ELIMU SEKONDARI, ELIMU MSINGI NA AFYA**

Kikao kilifahamishwa kwamba, Kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali kupitia Mpango wa Maendeleo ya Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya Uviko – 19, EP4R na Tozo ya Miamala imetoa fedha za kukamilisha miradi Nchini katika Sekta ya Elimu na Afya.

Kikao kiliendelea kuelezwa kuwa, Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo kupitia vyanzo hivyo katika Sekta ya Elimu imefanikiwa kupata kiasi cha **Tshs, 1,095,617,139.55** kwa utekelezaji wa miundombinu ya madarasa thelathini na saba (37) ya Shule za Sekondari na madarasa kumi na nne (14) ya Shule shikizi za Msingi na Sekta ya Afya imefanikiwa kupata kiasi cha **Tshs, 673,638,788/=** kwa mchanganuo ufuatao:-

| A: CHANZO CHA FEDHA: UVIKO - 19 | | | |
|---|---|---|---|
| **NA** | **MRADI** | **KIASI** | **MAELEZO** |
| 1 | Madarasa 37 ya Shule za Sekondari | 740,000,000.00 | Zimepokelewa |
| 2 | Madarasa 14 ya Shule shikizi za Msingi | 280,000,000.00 | Zimepokelewa |
| 3 | Ujenzi wa jengo la dharula (EMD) | 300,000,000.00 | Hazijapokelewa |

| NA | MRADI | KIASI | MAELEZO |
|---|---|---|---|
| 4 | Ujenzi wa Nyumba ya Watumishi wa Sekta ya Afya | 90,000,000.00 | Hazijapokelewa |
| 5 | Uhamasishaji Uviko – 19 (Hospitali ya Wilaya) | 33,638,788.00 | Zimepokelewa |
| | **JUMLA UVIKO – 19** | **1,443,638,788.00** | |

**B: CHANZO CHA FEDHA: EP4R**

| NA | MRADI | KIASI | MAELEZO |
|---|---|---|---|
| 1 | Ujenzi wa mifumo ya SWASH | 35,617,139.55 | Zimepokelewa |
| | Ujenzi wa madarasa mawili Shule ya Msingi Zinga | 40,000,000.00 | Zimepokelewa |
| | **JUMLA EP4R** | **75,617,139.55** | |

**C: CHANZO CHA FEDHA: TOZO ZA MIAMALA YA SIMU**

| NA | MRADI | KIASI | MAELEZO |
|---|---|---|---|
| 1 | Ujenzi wa Kituo cha Afya Fukayosi | 250,000,000.00 | Zimepokelewa |
| | **JUMLA MIAMALA YA SIMU** | **250,000,000.00** | |
| | **JUMLA KUU: A + B + C** | **1,769,255,927.55** | |

Kikao kiliendelea kufahamishwa kuwa, Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo imeshaingiziwa vifungu katika mfumo wa Mpango na Bajeti ulioboreshwa (Improved Planrep) kwa ujenzi wa madarasa ya Elimu ya Uviko – 19 na fedha ya Kituo cha Afya Fukayosi iko tayari kwa ujenzi.

## 01: MUDA WA UTEKELEZAJI:

Katika jitihada za kukamilisha utekelezaji wa miradi hii kwa wakati, Serikali imetoa maelekezo mahususi kuhusiana na muda wa kukamilisha utekelezaji wa miradi hii kama ifuatavyo:-

01: Miradi ya ujenzi wa vyumba vya madarasa na ofisi za Walimu zitatakiwa kutekelezwa na kukamilika katika kipindi cha Oktoba hadi 15 Desemba, 2021

02: Mradi wa ujenzi wa Kituo cha Afya Fukayosi unatatakiwa kutekelezwa na kukamilika katika kipindi cha Oktoba, 2021 hadi Januari, 2022

**B: Mapendekezo kwa ajili ya Ujenzi wa Mifumo ya Kunawia ni kama ifuatavyo:-**

| NA | KATA | JINA LA SHULE | KIASI CHA FEDHA |
|---|---|---|---|
| 1 | MAKURUNGE | SHULE YA MSINGI BIGILO | 11,872,379.85 |
| 2 | MAGOMENI | S/MSINGI KIDONGOCHEKUNDU | 11,872,379.85 |
| 3 | FUKAYOSI | SEKONDARI YA FUKAYOSI | 11,872,379.85 |
| | **JUMLA KUU** | | **35,617,139.55** |

**03: MPANGO MKAKATI (STARATEGIES) WA UKAMILISHAJI WA MIRADI**

01: Ujenzi wote wa miradi ya Elimu Msingi, Sekondari na Afya utatekelezwa kwa njia ya Force Account

02: Kuitisha Kikao Kazi na Wadau wote watakaoshiriki katika utekelezaji wa miradi hii. Kikao kazi hiki kimeshafanyika tarehe 15/10/2021 na ilikuwa ni kwa ajili ya kutoa maelekezo na kuweka Mpango wa pamoja wa utekelezaji kwa Halmashauri ya Bagamoyo

03: Mipango kazi ya utekelezaji wa miradi husika imeandaliwa kwa kuzingatia muda wa utekelezaji uliopangwa

04: Kuundwa kwa Kamati mbalimbali za usimamizi na ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi, kwa ngazi ya Halmashauri na ngazi ya chini. Kwa upande wa ngazi ya Halmashauri timu ya Wajumbe 12 imeshaundwa inayojumuisha Wakuu wa Idara na Vitengo vya H/Wilaya kama ifuatavyo:-

| NA | JINA | CHEO | IDARA/KITENGO |
|---|---|---|---|
| 1 | Aloysi Kaziyareli | DSEO | Elimu Sekondari |
| 2 | Wema Kajigili | DPRO | Elimu Msingi |
| 3 | Dr. Lugano Mwakipesile | AG. DMO | Afya, |
| 4 | George Mwalukasa | DHRO | Utumishi na Utawala |
| 5 | Maldboard Kapinga | DPLO | Mipango, |
| 6 | Lusingi Mashashi | AG. DE | Ujenzi, |
| 7 | Hemedi Malogo | DLO | Sheria, |

| NA | JINA | CHEO | IDARA/KITENGO |
|---|---|---|---|
| 8 | Daniel Pangani | DLDFO | Mifugo na Uvuvi |
| 9 | George Mzeru | DTR | Fedha na Biashara |
| 10 | Arstarico Nteye | HPMU | Manunuzi na Ugavi. |

Kwa upande wa Kamati ya ngazi za chini Kamati tatu zimeundwa kwa mujibu wa Mwongozo wa 'Force Account, Kamati hizo ni Kamati ya Ujenzi, Kamati ya Manunuzi na Kamati ya Mapokezi ya vifaa vya ujenzi:-

01: Ununuzi wa vifaa vya ujenzi ***"Bulk Procurement"*** ya vifaa kama nondo, mabati, mbao na square pipes unatarajiwa kutumika

02: Ufuatiliaji wa mara kwa mara kupitia Kamati ya Usimamizi ya Halmashauri

03: Kushirikisha Viongozi wa ngazi ya Vitongoji, Vijiji, Kata na Wananchi kwa ujumla kwa kutumia dhana ya fursa na vikwazo kwa Maendeleo iliyoboreshwa (Improved O&OD) ili kuwa na umiliki na uendelevu wa miradi husika. Hatua ambayo imeshaanza kutekelezwa na ushiriki wa Wananchi unakuwa mkubwa katika utekelezaji wa miradi

04: Kuridhiwa kwa malipo ya fundi na kufanyika malipo kwa wakati ili kukamilisha mradi kama ilivyopangwa kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Miongozo iliyopo

05: Kutenga gari maalum SM 9133 litakalotumika kusimamia miradi

Kikao kiliipokea Taarifa hiyo na kuijadili kwa kupitia kipengele kwa kipengele ambapo Wajumbe wa Kikao cha Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango waliipongeza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Hassan Suluhu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuhakikisha huduma za Elimu na Afya zinaboreshwa katika Nchi ya Tanzania.

Aidha kukamilika kwa vyumba vya madarasa katika Shule za Msingi na Sekondari kutasaidia kutatatua changamoto ya mlundikano wa Wanafunzi darasani na kuwezesha mazingira ya kujifunza kuwa bora zaidi sambamba na kuboresha huduma za Afya kwenye maeneo ya kutolea huduma za Afya, kisha Wajumbe kwa pamoja walifikia makubaliano kuwa;-

**MAKUBALIANO:**

01: Wajumbe wa Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango. wote kwa pamoja waliipokea taarifa ya Mapokezi ya fedha kiasi cha **Tshs, 1,769,255,927.55** za Miradi ya Maendeleo kutoka Serikali Kuu kwenda Sekta ya Elimu na Afya kuwa ni taarifa sahihi ya mapokezi ya fedha hizo kama ilivyowasilishwa

02: Idara za Elimu Msingi, Sekondari na Afya kwa kushirikiana na Idara ya Ujenzi wasimamie ujenzi wa miradi hii kwa kila hatua ili hatimaye miradi inayojengwa iwe na kiwango/ubora unaotakiwa.

03: Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi asimamie na kuhakikisha shule zote zilizopatiwa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa vyumba vya madarasa wanatekeleza miradi hii kwa kuzingatia Sheria na Kanuni za Manunuzi ya Umma sambamba na Mwongozo wa 'Force Account'

04: Taarifa ya Mapokezi ya Fedha kiasi cha **Tshs, 1,769,255,927.55** za miradi ya maendeleo kutoka Serikali Kuu kwenda Sekta ya Elimu na Afya iwasilishwe kwenye Mkutano wa Baraza la Madiwani ujao

**MUHT.NA.HWB/FUM/05/82/2021/2022 - TAARIFA YA IDADI YA MAJENGO YATAKAYOJENGWA KATIKA KITUO CHA AFYA FUKAYOSI**

Kikao kilifahamishwa kwamba, Halmashauri ya Wilaya Bagamoyo imepokea barua yenye Kumb. Na. CFC.133/307/01.LL/89 ya tarehe 28/10/2021 kutoka OR – TAMISEMI ikiwa ni malekezo ya ujenzi wa Vituo vya Afya 60 kwenye Tarafa zisizo na Vituo vya Afya pamoja na Kata za kimkakati.

Katika barua hiyo yapo maelekezo kwamba ujenzi wa Vituo vya Afya awamu ya pili utahusisha ujenzi wa majengo mawili yakiwemo jengo la Wagonjwa wa nje (OPD) na jengo la Maabara (Labaratory).

Kwa upande wa Halmashauri ya Wilaya Bagamoyo, ilipanga kujenga majengo mawili ya Wodi ya Akina Mama Wajawazito na Jengo la Upasuaji, hii ni kutokana na Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo kuchangia ujenzi wa Wagonjwa wa nje (OPD) na jengo la Maabara (Labaratory).

Aidha eneo hili la Zahanati ya Fukayosi limeelekezwa kujengwa Kituo cha Afya kwa kuwa ndiyo eneo lililokidhi mahitaji ya ukubwa kwani lina ukubwa wa ekari tano (5) zinazotosheleza ujenzi huo.

Aidha Kata ya Fukayosi ina jumla ya wakazi wapatao 14,812 wakiwemo Wanaume 7692 na Wanawake 7118 ikiwa na jumla ya kaya 4168 na jengo hili lipo njia kuu kutoka Dar es Salaam kwenda Msata kupitia Bagamoyo kwa ujenzi huo Wananchi wa Kata ya Fukayosi na Kata mbili za jirani za Makurunge na Kiwangwa wote wanategemea kupata huduma ndani ya Kituo hicho.

Kikao kiliipokea Taarifa hiyo kisha Wajumbe waliijadili, katika kuijadili taarifa hiyo Wajumbe walipata nafasi ya kuhoji hoja mbalimbali na kupatiwa ufafanuzi

Kikao kiliipokea taarifa hiyo, kisha Wajumbe waliipongeza Serikali kwa kutoa kibali cha ajira kwa Mtaalam wa Mionzi katika Halmashauri ya Wilaya Bagamoyo kwa maana ya Hospitali yaa Wilaya na hasa kwa kuzingatia kuwa ilikuwa ni tatizo kubwa kwa Hospitali ya Wilaya kukaa bila Mtaalam wa mionzi kwa muda mrefu sasa.

Hivyo Wajumbe walisisitiza kwa Idara ya Utumishi na Utawala kusimamia na kuhakikisha taratibu za kuajiriwa kwa Mtaalam huyo wa Mionzi zinakamilka ndani ya muda ulioelekezwa. Wajumbe kwa pamoa walifikia makubaliano kuwa;

**MAKUBALIANO:**

01: Wajumbe wa Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango wote kwa pamoja waliipokea taarifa hiyo kuwa ni taarifa rasmi ya kupokelewa kwa Kibali cha Ajira ya Mteknolojia Drj II (Mionzi) katika H/Wilaya Bagamoyo

02: Taarifa ya kupokelewa kwa Kibali cha Ajira ya Mteknolojia Drj II (Mionzi) katika H/Wilaya Bagamoyo iwasilishwe kwenye Mkutano wa Baraza la Madiwani ujao

**MUHT.NA.HWB/FUM/05/98/2021/2022 - KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti aliwashukuru Wajumbe na Wataalam kwa michango yao waliyoitoa katika Kikao hicho. Aidha alisisitiza Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W) kutekeleza maagizo/maazimio yanayotolewa kwenye vikao kwa wakati na kwa usahihi ili hatimaye Wajumbe kupokea utekelezaji unaojitosheleza kwa lengo la kuboresha na kuleta ufanisi katika shughuli mbalimbali za Halmashauri.

Kikao kilifungwa mnamo saa 11.40 jioni

**U M E T H I B I T I S H W A**

| | |
|---|---|
| ............................................ | ............................................ |
| *Shauri, Selenda* | *Mohamed A. Usinga* |
| **MKURUGENZI MTENDAJI (W)** | **MWENYEKITI** |
| **KATIBU** | **HALMASHAURI YA WILAYA** |

**TAREHE........................**